**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**


**Namba za Simu;**
**Mkuu wa Shule** **<u>0767668617</u>**
**Makamu Mkuu wa Shule ;0626815554**
**Matron/Patron** **<u>0622490619/ 0766038043</u>**

**Shule ya Sekondari Rusumo**
**S.L.P 50**
**Ngara**
**…………………**


**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

**YAH: <u>MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI RUSUMO, HALMASHAURI YA NGARA MKOA KAGERA MWAKA ..........</u>**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka **.........** na atasoma tahasusi ya …………Shule ya Sekondari **RUSUMO** ipo umbali wa Kilometa **34** Kaskazini/Kusini/Mashariki/Magharibi mwa Mji wa NGARA. Shule ipo eneo linaitwa BENACO ni karibu sana na barabara, kwa wanafunzi wanaotokea maeneo ya mwanza, Bukoba, Karagwe, Shinyanga, Geita, Biharamulo washukie katika kituo cha mabasi BENACO. Kutoka kituo hicho shule ipo umbali wa **KM 1** barabara ya kuelekea Karagwe. Usafiri kwa pikipiki ni Shilingi 1000/= hadi shuleni. Muhula wa Masomo unaanza tarehe **..................** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **..............** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **……………..**

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

2.1 **Sare za Shule**

- **Kwa upande wa wasichana**
  Sare ya shule hii ni Siketi mbili nyeusi kitambaa kizito malinda ya kuelekea upande, upande wa malinda uwe inchi mbili, sketi iwe na urefu wa kutosha ifike kwenye kifundo cha mguu(Ankle) na michirizi miwili meupe upande wa mbele.
- **Kwa upande wa wavulana**
  Sare ya shule hii ni Suruali mbili nyeusi vipimo upana wa inchi 19-21 iwe na mfuko mmoja nyuma, modo hazruhusiwi kabisa kwa Wavulana.

i. Mashati rangi nyeupe mikono mirefu
ii. Rangi ya Hijab (kijuba) ni Nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama.
iii. Sare ya michezo ni (Bukta, T – Shirt na socks) za kampuni ya ADIDAS/SPORTS (T – shirt isiwe na maandishi yoyote tofauti na nembo ya kampuni ya Adidas/Sports) pamoja na Track suit ya blue kampuni ya Adidas/sports, Raba za michezo. Vitavaliwa wakati wa michezo uwanjani

tu. Rangi ya Bukta, T – shirt na soksi inatokana na Tahasusi uliyopangiwa kwa mchanganuo ufuatao:-

- PCB – Blue
- CBG – Rangi nyeusi
- HKL – Rangi ya Machungwa
- HGL – Kijani
- HGLi – Njano
- HGFa – Nyekundu

iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
v. Soksi jozi mbili nyeupe (stocking) kwa wasichana na nyeusi kwa wavulana za shule;
vi. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;
vii. Sweta rangi ya kijani jeshi kwa wasichana na wavulana.
viii. Nguo za kushindia;Suruali rangi ya damu ya mzee mbili kwa wavulana na sketi mbili rangi ya damu ya mzee kwa wasichana; (NB, Zingatia aina ya vipimo vilivyoainishwa.), Sweta moja rangi ya zambarau kwa wasichana na wavulana.
ix. Tai nyeusi nyenye michirizi meupe midogomidogo. (ukiikosa itaweza kupatikana kwenye duka la shule kwa Tsh 5,000/=)
x. Tisheti (T-shirt) rangi ya blue yenye kola kwa wasichana na wavulana yenye muhuri wa shule.(ukiikosa itaweza kupatikana kwenye duka la shule kwa Tsh 15,000/= ili kuleta ufanano)

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari 12 (COUNTER BOOK QUIRE 4) na kalamu za kutosha
ii. Ream (A4) mbili za karatasi aina ya **DOUBLE A** kwa mwaka
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (orodha imeambatanishwa)
iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;
v. Scientific Calculator;(wanaosoma masomo ya sayansi)
vi. Godoro liwe na vipimo vya 2 na nusu kwa sita.
vii. Mashuka Jozi 2 rangi ya blue, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 rangi ya blue.
viii. Nguo za ndani za kutosha;
ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
x. Mwanafunzi aje na vifaa vifuatavyo kulingana na Tahasusi yake:-

| **TAHASUSI** | **KIFAA** |
|---|---|
| PCB | Kwanja lililonolewa, mopa, hardbrush |
| CBG | Kwanja lililonolewa, mopa, kotama |
| HKL | Kwanja lililonolewa, mopa, jembe lenye mpini |
| HGL | Mopa, panga, mfagio wa nje (chelewa) |
| HGLi | Mopa, soft Broom, Panga |
| HGFa | Kwanja lililonolewa, mopa, mfagio wa nje (chelewa) |

**2.3 Michango mbalimbali**

**a) Shule za Bweni**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 2. | Tahadhari | 5,000/= |
| 3. | Nembo | 5,000/= |
| 4. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**NB: MICHANGO HII IWEKWE KWENYE AKAUNTI YA SHULE NA 32101200059 NMB JINA LA AKAUNTI - RUSUMO SECONDARY SCHOOL**

***(Tafadhari andika jina la mwanafunzi kwenye pay slip na kuja nayo shuleni).***

# SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

## 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalumu toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).**

## 3.2 MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE NI PAMOJA NA:

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;

xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

3. **Viambatisho na Fomu Muhimu**
   **TANIBIHI:**
   a) Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
   b) Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
   c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
   d) Afike na result slip na cheti cha kuzaliwa
   e) Lazima aje na kadi ya bima ya Afya ya mwanafunzi inayotolewa na NHIF (Shirika la Taifa la Bima ya Afya) au shilingi 50,400/=
   f) Abandika picha nne (4) za wazazi au ndugu wa karibu pamoja na namba zao za simu wanaoweza kutembelea mwanafunzi na kushirikiana na shule katika malezi
4. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**
**KARIBU SANA RUSUMO**



**GODFREY BRAYAN**
**MKUU WA SHULE**




**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. Tafadhali upatapo ujumbe wowote kuhusu mwanafunzi/mtoto wako usitume chochote, ni vema ukawasiliana na uongozi wa shule kupata ukweli wa taarifa husika kwa namba zifuatazo: -**

- **Mkuu wa shule 0767668617**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0626815554**
- **Mwandamizi Taaluma 0753641926/0717589829**
- **Mwandamizi Malezi 0743466503**

**ORODHA YA VITABU VYA MASOMO WANAVYOTAKIWA KUNUNUA WAZAZI**

Vifuatavyo ni vitabu vitakavyomsaidia mwanao kwa masomo husika kati ya vilivyoorodheshwa hapa chini:-

**HISTORIA**

1. History for Secondary Schools Form five (Tanzania Institute of Education)
2. History for Secondary Schools Form Six (Tanzania Institute of Education)

**ORODHA YA VITABU VYA KISWAHILI, ENGLISH, LITERATURE IN ENGLISH NA FASIHI YA KISWAHILI**

**Novel (English)**

- Animal Farm by George Orwell
- Chasing the Leopard Finding the Lion by Julie wakeman linn
- The opportunist Elite by Nyambari C. M Nyangwine
- The Horizon Unveiled by Fellowes Mwaisela

**Play (English)**

- The Government Inspector By Nikolai V. Gogol
- An Enemy of the People by Henrik Ibsen
- A Taste of Heaven by Farouk Topan

**Poetry (English)**

- Summons: Poems from Tanzania by Richard S. Mabala et al.
- Poets of Africa: Lament of the Silent & Other Poems

**Novel (Literature in English)**

- Arrow of God by Chinua Achebe
- A man of the People by Chinua Achebe
- A Grain of wheat by Ngugi wa Thiong’o
- Petals of Blood by Ngugi wa Thiong’o
- No longer at Ease by Chinua Achebe
- Joy Comes In the Morning by Hopolang Phororo
- The Lion of Yola by Severine Ndunguru

**Play (literature in English)**

- Betrayal in the City by Francis Imbuga
- I will mary when I want by ngugi wa Thiong’o & Ngugi wa Mirii
- Julius Caesar by William Shakespeare
- Man of Kafira by Francis Imbuga

**Poetry (Literature in English)**

- Poets of Africa 7; Boundless voices poem from Kenya by Arthur I. Luvai
- The bleeding Heart and other Poems by Shilia Kaaya

**Riwaya (Kiswahili)**

- Dunia uwanja wa Fujo – Euphrase Kezilahabi
- Ua la Faraja – W.E.Mkufya
- Mirathi ya Hatari – C.G.Mung’ong’o
- Wasifu wa Siti Binti Saad – Shaaban Robert

**Tamthiliya (Kiswahili)**

- Mukwava wa uhehe – M.M.Mulokozi
- Shujaa Mirambo – Emmanuel Mbogo
- Usaliti Mjini – Francis Imbuga

**Ushairi (Kiswahili)**

- Fumbo linaloelea – Nyambari C.M.Nyangwine
- Malenga wa ziwa Kuu – wallah Bin Wallah
- Andamo, Msafiri safarini – Mohammed khelef Ghassani

- Wosia wa baba – Ahmed Mohamed Amanzy

**Riwaya (Fasihi ya Kiswahili)**
- Vuta N'kuvute – shafi Adam Shafi
- Asali Chungu – Said Ahmed Mohamed
- Mwana wa Yungi Hulewa – Mohammed Said Abdulla
- Vipuli vya Figo – Emmanuel Mbogo

**Tamthiliya( Fasihi ya Kiswahili)**
- Kaptula la Marx – Euphrase Kezilahabi
- Nyerere na safari ya Kanaani – Emmanuel Mbogo
- Morani – Emmanuel Mbogo

**Ushairi (fasihi ya Kiswahili)**
- Dhifa – Euphrase Kezilahabi – Euphrase Kezilahabi
- Utenzi Mjumui wa Karne ya 21 - Idd M. Mwimbe
- Malenga wa Bara – M.M.Mulokozi na K.K. Kahigi
- Fungate ya Uhuru – Mohamed seif Khatibu

**CHEMISTRY**
- General and organic chemistry for Advanced level (TIE)
- Physical chemistry for advanced level (TIE)
- Organic chemistry for advanced level (TIE)

**BIOLOGY**
- Biology for advanced secondary schoos, student's book form five (TIE)

**PHYSICS**
- Physics for Advanced secondary (TIE)

**BASIC APPLIED MATHEMATICS**
- Basic applied mathematics (TIE)

**GEOGRAPHY**
- Practical Geography for Advanced secondary schools student's Book (TIE)
- Physical Geography for advanced secondary schools student's book

**NGARA DISTRICT COUNCIL**

Rusumo Secondary School,
P.O.Box 50,
**Ngara .**
Date……………………….

To Medical Officer,
………………………
………………………
………………………
………………………

**Ref ........................................................................................*(Name of student)***
Please examine the above named student as per Medical examination form below:

………………………..
**HEADMASTER**

MEDICAL EXAMINATION FORM
**(*To be completed by Government Medical Offer)*** Full Name:
……………………………………………………………………………
Age: ……………………………Height:…………(cm)Weight ........ (kg)

1. Blood count:………………………………………………………………….
2. Stool Examination:…………………………………………………………
3. Urinary:…………………………………………………………………….
4. STDs and other V.D:……………………………………………………….
5. TB and Leprosy test:……………………………………………………….
6. Eye Test:……………………………………………………………………
7. Ear Test:…………………………………………………………………….
8. Chest:……………………………………………………………………….
9. Abdomen:…………………………………………………………………..
10. Spleen:………………………………………………………………………

Any additional information:
E.g Physical defects or impairments, infections, chronic or family diseases (Eg. Sickle cell), in ability to eat certain foods etc
……………………………………………………………………………………………….
……………………………………………………………………………………………….
………………………………………………………………………………………………
I have examined the above named student and I certify that He/She is FIT/NOT FIT to pursue Secondary Education.

………………………………….. ………………………
Signature and Official Stamp Date
Station:………………………… Designation:……………..

**MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI**

1. Jina kamili ……………………………………………… (*kama ilivyo kwenye form four SEL form na Birth Certificate*)
2. Tarehe ya kuzaliwa …………………………… Anwani ya Nyumbani……………………………………
3. Mahali unapoishi (Nyumbani kwenu): Wilaya…………….Tarafa………………… Kata…………………….. Kijiji………………………………
4. Shule ya Sekondari ulikotoka…………………………………Anwani …………………………………
5. Dini…………………………………………………………………………….
6. Kabila…………………………………………………………………………
7. Taifa (*Mtanzania/si Mtanzania*)…………………………………………………
8. Jamaa katika familia: (*Watakaohusishwa katika malezi ya mwanafunzi akiwa hapa shuleni*)

i. Jina la Baba…………………………………………..
Anwani……………………………SIMU NA.1……………….Anaishi/Haishi ……………… 2……………….Kazi yake………………………

| |
|---|
| Picha ya Baba Mzazi |

ii. Jina la Mama……………………………………………..
Anwani……………………………SIMU NA.1……………….Anaishi/Haishi ………………… 2……………….Kazi yake……………………

| |
|---|
| Picha ya Mama Mzazi |

iii. Jina la Mlezi……………………………………………..
Anwani……………………………SIMU NA.1……………….Kazi yake…………………… 2……………….Uhusiano wake na wewe…………………

| |
|---|
| Picha ya Mlezi/Ndg. wa karibu |

iv. Jina la Mlezi……………………………………………..
Anwani……………………………SIMU NA.1……………….Kazi yake………………… 2……………….Uhusiano wake na wewe………………………..

| |
|---|
| Picha ya Mlezi/Ndg. wa karibu |

v. Idadi ya Kaka……………………………………………
vi. Idadi ya Dada……………………………………………
vii. Wewe ni wa ngapi katika familia…………………………

Mimi (*Mwanafunzi*)nathibitisha kuwa taarifa nilizozijaza hapo juu ni za kweli.

……………………………………..            ……………………………
Sahihi ya Mwanafunzi                          Tarehe

Mimi …………………………………(*Mzazi/Mlezi*) wa Mwanafunzi …………………………… nimehakikisha kuwa taarifa zilizojazwa hapo juu ni za kweli.

……………………………….            ……………………………………………..
Sahihi ya Mzazi/Mlezi                          Tarehe

Jina la Afisa Mtendaji wa Kijiji/Mtaa ……………………………………………… Sahihi ya Afisa Mtendaji wa Kijiji/Mtaa…………………………………….. Tarehe………………… Simu Na:1…………………………, 2……………………., 3…………………

Anwani……………………………..
……………………………………..
……………………………………..
……………………………………..
Tarehe………………………………

Mkuu wa Shule,
Shule ya Sekondari Rusumo,
S.L.P 50,
NGARA.

**YAH: KUKUBADILI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI RUSUMO**

Mimi ......................................................................... (Jina la Mwanafunzi) nimepokea barua ya kuchaguliwa kujiunga na kidato cha TANO katika shule ya /sekondari Rusumo kuanzia mwaka………………………………… ****Nakubali/Sikubali*** nafasi hiyo. Nimesoma na kuelewa Sheria na Masharti ya kujiunga na shule hii yaliyoambatanishwa. Hivyo ninaahidi kujifunza kadri ya uwezo wanfu wote bila kupoteza muda au kufanya mzaha wowote kama Sheria zilivyo ainishwa. Nitatimiza wajibu wangu wote kwa muda na wakati uliopangwa. Pia ninaahidi kuwa nitatii sheria zote za shule. Endapo nitashindwa kutii na kufuata Sheria hizo hatua zinazostahili zichukuliwe dhidi yangu. Natoa ahadi hizi mbele ya Mzazi/Mlezi wangu, ambaye naye ametia sahihi yake kwenye kifungu kinachofuata chini.

…………………………………………………….. ………………………………..
SAHIHI YA MWANAFUNZI TAREHE

Mimi ..............................................................................(*Jina la *Mzazi/Mlezi*)
*Nakubali/Sikubali mtoto wangu ajiunge na Shule ya Sekondari Rusumo. Nimesoma na kuelewa sheria na masharti ya kujiunga na Shule hii. Hivyo nakubaliana na masharti na sheria hizi ambazo itambidi mwanangu azifuate kama alibyoahidi mbele yangu. Nipo tayari kulipa Ada na michango yote. Nitashirikiana na uongozi wa shule pamoja na jumuiya nzima ya shule katika kutoa malezi bora kwa mwanangu kulingana na sheria za shule na matakwa ya Taifa kwa ujumla.
Taarifa na mawasiliano yote yahusuyo mwanangu yatumwe kwangu kwa kutumia anwani ifuatayo
………………………………………..
………………………………………..
………………………………………..
……………………………………….. Namba za simu: …………………………
…………………………
………………………… Mabadiliko
yoyote ya anwani yangu nitayatuma kwa Mkuu wa shule kwa maandishi

Sahihi ya * *Mzazi/Mlezi*……………………………….. Tarehe ………………………………..

****Futa isiyotakiwa***




RUSUMO SECONDARY SCHOOL
NGARA - KAGERA
DISCIPLINE TO ACADEMIC EXCELLENCE



